

Mbali na kodi, Watanzani wanakwazwa na sheria inayowataka kumiliki magari kama haya matano ndipo wasajili makampuni ya utalii.



Kodi na tozo lukuki zinalalamikiwa kuwa chanzo cha kuwaengua Wazanzibari wazawa kumiliki hoteli za kitalii kama hii.

# Tozo, kodi zakwamisha juhudi za kujikomboa kiuchumi

**Na Beda Msimbe**

MMILIKI wa nyumba ya kulala wageni ya Malindi, Marisa Yusuf anaona ni heri sasa aachane na biashara ya hoteli na kufanya kitu kingine kutokana na kutopata faida katika kazi hiyo.

Kukosekana kwa faida hakutokani na kushindwa 'kulisha' wateja wake bali kunatokana na tozo nyingi anazokatwa na mamlaka mbalimbali ambazo zinafanya kazi yake ya hoteli kuwa mchezo wa kuigiza.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi katika hoteli yake iliyopo Mji Mkongwe, Yusufu anasema kwamba maamuzi yake ya kuachana na kuendesha hoteli hiyo ambayo kwake ni urithi ni kunatokana na mamlaka husika kutokuwa tayari kusikiliza matatizo yanayoambatana na tozo zaidi ya tano katika biashara moja.

Marisa anasema anatozwa fedha katika Mji Mkongwe, analipa ushuru wa hoteli, analipa kodi ya mapato, analipa leseni.

"Kuwa Mji Mkongwe pekee kunafanya nilipe tozo zaidi ya tatu na ukiwaeleza kwamba msimu mbaya wanaokuelewa na kukuelekeza ni TRA pekee, lakini si mamlaka nyingine," alisema Marisa kwa masikitiko.

Lalamiko la tozo nyingi halikuwa kwa mfanyabiashara huyo pekee, lakini waandaaji wa Tamasha la Filamu la Kimataifa la Zanzibar (ZIFF) nao walilalamikia tozo nyingi zinazowafanya wakose pumzi na kushindwa kufanya mambo mengine ambayo yangeliwasaidia Wazanzibari wenyewe na taifa kwa ujumla.

"Unajikuta lazima ulipe tozo mbalimbali na matokeo yake hata kuwaita watu wengi zaidi ili kunufaisha watanzania katika kuhamisha elimu haiwezekani," anasema Mweneja wa Tamasha, Daniel Nyalusi.

Mfanyabiashara mwingine wa masuala ya teknohama, Joseph Mwale anasema kutokana na mazingira mabovu ya tozo kuanzia leseni hadio mapato na mahali unapoendeshea shughuli, watu wanajitahidi kuwakwepa wataalamu ili angalau kupata faida kidogo.

"Kwa kuwa mimi hapa kwetu hainisaidii sana kwani mazingira ya tozo hayakupi nafasi ya kupumua," anasema na kuongeza kwamba kama angelikuwa si mkazi wa hapa angelijaribu kutafuta njia nyingine ya kuishi lakini si biashara ya teknohama ambayo sasa anaiona inakula hadi mtaji wake.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Zanzibar (ZNCCIA), Mbarouk Mohamed, katika mazungumzo yake anasema tozo nyingi zilizopo katika mfumo wa biashara Zanzibar zinawanyima wazawa kupanuka kibiashara.

"Sijui wenzetu huko bara mkoje, lakini hapa ni tatizo kidogo na tupo katika mazungumzo na serikali kuona namna ya kupunguza kodi ili wafanyabiashara wapumue," anasema mwenyekiti huyo.

Anasema taasisi yake imefanya utafiti ambao upo tayari kuchapishwa, utafiti ambao umeonesha wazi kwamba mazingira ya kufanyabiashara Zanzibar ni magumu kutokana na wingi wa tozo na pia kodi inayozidi asilimia 50 maeneo mengine.

Aidha anasema kwa wafanyabiashara wa Zanzibar, kodi ni mtihani mkubwa kwani inalamba hadi mtaji. Pia anasema kwamba nyingi ya tozo na hata leseni zimegeuzwa kuwa chanzo cha kodi na matokeo yake inaharibu kabisa nia njema ya leseni na hata kanuni zake.

Anasema mazungumzo wanayoendelea kufanya na serikali na hasa baada ya utafiti kubainisha kuwapo kwa mazingira mabaya ya kodi na hivyo wafanyabiashara kushindwa kuendelea yamelenga kuishawishi serikali si tu kupunguza kodi ila pia na kuhakikisha kwamba leseni hazitumiki kama kodi.

"Kodi zinatakiwa kuwa endelevu kama unatoza kodi na biashara inakufa haina maana," anasema mwenyekiti huyo na kutoa wito kwa mamlaka husika kuangalia pia namna ya kuwezesha wafanyabiashara kuwa na mazingira mazuri ya kazi zao ili waweze pia kujiendeleza.

Mohamed anakiri kwamba kuna tozo nyingi Zanzibar ambazo zinakwamisha biashara kuwa endelevu na tozo hizo ambazo zimegawanyika wakati mwingine hata hazieleweki zinafanya nini na badala yake inafanya huduma zinazotolewa kuwa ghali.

Kwa taifa la Zanzibar ambalo nusu ya mapato yake yanategemea biashara ya utalii, tozo zinazotolewa zinaleta shida kubwa kwa wajasiriamali hasa wazalendo.

Kwa mujibu wa Mohamed, utafiti ambao wameufanya unaonesha kudorora kwa wajasiriamali kutanua shughuli zao na pia kunyima fursa za kuweka akiba kwa ajili ya maendeleo.

"Tunaendelea kuzungumza na serikali kuhusu hili kwani lipo hata kwenye utafiti. Huwezi kuwa na tozo nyingi hivi halafu uitarajie sekta kuendelea na serikali kuchuma katika hilo," anasema kwa njia ya simu wakati akihojiwa.

Ingawa leseni zinatakiwa kutumika kama sehemu ya kurekebisha baadhi ya utaratibu, kuzuia au kuwezesha, tozo za Zanzibar kwa maoni ya taasisi ya wafanyabiashara zinachangia kukatisha tamaa wawekezaji wazawa, kama ilivyo kwa Marissa.

Wakati Wazanzibari wanalalamikia tozo nyingi zinazokwamisha uwekezaji na hata kutanua shughuli, wenzao wa Bara katika sekta ya utalii matatizo ni mengi zaidi na yote yanahusu kodi na utoaji wa leseni.

Katika hali isiyoangalia menejimenti ya utalii ya kisasa zaidi ufunguaji wa kampuni ya utalii ni balaa kutokana na kutakiwa kuwa na magari matano ya mkonga mapya.

Thamani ya magari hayo ambayo si chini ya Sh milioni 80 kwa gari moja kunafanya wazalendo kutokuwa na uwezo wa kuanzisha kampuni achilia mbali leseni lukuki anazotakiwa kuwa nazo mtu.

Fina Mwanambilimbi wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), anasema kwamba malalamiko makubwa ambayo yamefikishwa ofisini kwake ni leseni, tozo na kodi ambazo wafanyabiashara wa Tanzania wanaona zinawaua.

Anasema katika mazungumzo kutoka Arusha kwamba watanzania wanauliza mazingira ya uwekezaji ambayo yanawalinda zaidi wageni wenye pesa na kuwaacha wenyeji wakiwa katika hali mbaya.

"Unapomwambia mtanzania kwamba hawezi kupata leseni ya kampuni ya utalii mpaka awe na magari mapya matano si sawasawa. Huyu mtu anaweza kabisa kupata watalii na akakodisha gari kwa makampuni ya kukodisha magari na shughuli ikaendelea. Sasa hapo ulazima huu wa nini?" Anahoji.

Akizungumzia malalamiko ya kodi, Mwanambilimbi amesema yametawanyika sana, lakini ni dhahiri serikali inatakiwa kuchukua hatua kuangalia malalamiko haya na kuanzisha vikundi kazi vya kuyashughulikia.

Aidha anasema kupanda kwa kodi na tozo nyingine kwa ghafla kunafanya hata wafanyabiashara ya utalii wawe katika hali ngumu, kwani watalii wanapoambiwa kuna tozo fulani huwa hawaelewi hasa anapokuwa akikamilisha malipo yake kwa mujibu wa taarifa aliyokuwa nayo hapo awali.